# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA NANE

**17 APRILI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 17 APRILI, 2023

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**94. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini barabara ya Kibaoni, Endala, Endamariek hadi Endabash itajengwa.

**95. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itawalipa fidia Wananchi waliohamishwa kupisha maegesho ya malori eneo la Kurasini tangu Mwaka 2015.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**96. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutimiza masharti ya ajira kwa Watumishi ikiwemo kuwapandisha madaraja na stahiki zingine.

**97. MHESHIMIWA AMINA DAUD HASSAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kuna mpango gani wa kufuatilia miradi ya TASAF iliyokamilika ili kuhakiki uendelevu wake.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**98. MHESHIMIWA MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI (CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukijenga upya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**99. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Sheria za Tanzania zinasema nini kuhusu mahusiano ya jinsia moja.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**100. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itaboresha bei ya ardhi inayotwaliwa na Migodi ili iendane na thamani ya ardhi ya eneo husika.

**WIZARA YA NISHATI:**

**101. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, nini matokeo ya utafiti wa mafuta uliofanyika katika Ziwa Tanganyika na lini mafuta yataanza kuchimbwa.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**102. MHESHIMIWA GEOFFREY IDELPHONCE MWAMBE (MASASI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza Ujenzi wa Stendi Mpya ya Mji wa Masasi ikiwa ni Mradi Funganishi wa Ujenzi wa Barabara ya Masasi hadi Mnivata.

**103. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Wananchi wa Kata ya Sitalike waliopisha ujenzi wa barabara ya Sitalike hadi Mpanda Hotel watalipwa fidia.

## WIZARA YA KILIMO:

**104. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini kimesababisha mbolea kuadimika na kuleta hasara kwa Wakulima na Wawekezaji nchini katika msimu wa Mwaka 2022/2023.

**105. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mapitio ya kubaini madawa na viatilishi vinavyosababisha madhara na vinaendelea kutumika katika Kilimo.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**106. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mkakati gani wa kuondoa tofauti ya Viwango vya Ufaulu kwa Mitihani ya Kidato cha Nne na Sita Kati ya Bara na Zanzibar.

**107. MHESHIMIWA SHANIF MANSOOR JAMAL (KWIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Chuo cha VETA Ngudu Kwimba kitakamilika.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**17 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**